**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA

Simu MKUU WA SHULE: +255 686756071

KICHEBA HIGH SCHOOL

S.L.P 58

MUHEZA

Tarehe……………………………

E-mail: kichebasecondaryschool@gmail.com

Makamu MKUU WA SHULE 0716823900

Malezi: 0610128694

Kumb Na. KHS/ ADM /JI/…………….

Mzazi/Mlezi wa ........ …………........................................................kidato cha.................……………….

2026 S.L.P ………………

**<u>YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KICHEBA HIGH HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA. MKOA WA TANGA MWAKA WA MASOMO …………………..</u>**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka…………………… na atasoma tahasusi ya …….…… Shule ya sekondari KICHEBA HIGH ipo umbali wa kilometa kumi na mbili(12km) kutoka stendi kuu ya Mabasi MUHEZA, Usafiri wa taksi kutoka mjini MUHEZA unapatikana kwa nauli ya Shilingi 15,000/=; kwa pikipiki Shilingi 4000/= na kwa bajaji shilingi 10,000/= Muhula wa Masomo unaanza tarehe......................, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe.................Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………….

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA;hge,egm na hgl**

i. Sare ya shule hii ni mashati 2 meupe ya mikono mifupi yasiyobana na sketi 2 za kaki mshono wa malinda 12 zenye mifuko 2 mbele, Kwa wanaovaa Hijabu, rangi ya hijabu 2 ifanane na sare ya shule (Hijabu nyeupe) bila urembo wa aina yoyote ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama na sketi 2 za kaki mshono wa malinda 12 iwe ndefu kugusa kifundo cha mguu.

ii. Shamba dress. aje na magauni 2 ya draft nyekundu na nyeupe na refu mpaka kwenye kiwiko cha mguu na lisilo na marinda na wanaotumia hijabu (kijuba) ni rangi nyeupe.
iii. Sare ya shule kwa michezo ni track suit mbili dark blue. Na raba za michezo nyeupe.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi 4 nyeupe za shule jozi 2 nyeusi nzito za kuvaa usiku;
vi. Sweta rangi ya blue, linawezapatikana shuleni kwa bei 15,000 ukipenda.
vii. T-shirt aina ya Form Six rangi ya ugoro (unaweza kuipata shuleni kwa gharama ya shilingi 10,000 ukipenda).

ANGALIZO

Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani zaidi ya zilizotajwa hapo juu.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counter book 4 quire tisa (9) na daftari za kawaida za mazoezi angalau moja kwa kila somo;
ii. Ream tatu (A4 duplicating papers) za Karatasi kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Advanced mathematics, physical geography, practical geogaphy, human and economic geography, general studies na basic applied mathematics vinavyotolewa na TAASISI YA ELIMU TANZANIA); Hata hivyo mzazi anashauriwa kuwasiliana na walimu kabla ya kununua vitabu ili apatiwe ushauri wa vitabu vinavyofaa zaidi.;
iv. Scientific Calculator
v. Godoro 1 na foronya yake (futi 3 kwa 6) na Chandarua (Neti) kwa ajili ya kujikinga na Mbu rangi ya blue.
vi. Mto na foronya yake rangi ya njano.
vii. Shuka jozi 2 za njano.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko (za lita kumi);
xi. Aje na Bima ya NHIF
xii. Vifaa vya usafi:- Kwanja (HGE na HGL), jembe (HE, HGL na EGM), panga (EGM), fagio la Ndani (soft broom) (EGM) na la nje la mti (HE na HGL),

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Michango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Tunashauri ingiza kwenye akaunti ya shule ya sekondari Kicheba NMB Ac. Na. **41901200045** kwa usalama wa fedha husika. Aje na hati ya malipo (bank pay in slip) halisi yenye jina la mwanafunzi husika ya benki ya NMB aliyolipia michango tajwa hapo juu. HATUPOKEI FEDHA TASLIMU. Gharama ya huduma ya kwanza: Tsh 10,000/= (ilipwe kupitia akaunti ya shule)

**<u>SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII</u>**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

viii. Uvutaji wa sigara;

ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xi. Kusababisha mimba;

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;

xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4 Fomu muhimu za kujaza mwanafunzi aje nazo shuleni

I. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

II. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

III. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KICHEBA HIGH SCHOOL

…………………………………….

SAMIMU. B. ABDALLAH
MKUU WA SHULE

**FOMU YA KUKIRI KUJIUNGA NA SHULE** (Ijazwe na mwanafunzi)

Jina la mwanafunzi…………………………………….

S.L.P------------------------

Tarehe-------------------------------

MKUU WA SHULE,

KICHEBA HIGH SCHOOL,

S.L.P. 59,

MUHEZA.

YAH; FOMU YA KUKIRI UCHAGUZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO……………………………….

1. Ahsante sana, kunijulisha kuwa nimechaguliwa kujiunga na kidato cha tano shuleni hapo.
2. Ninatoa ahadi kutii sheria zote za shule ambazo nimezisoma na kuzielewa.
3. Ninakubali / sikubali nafasi hii niliyopewa na Taifa.
4. Niko tayari kutimiza maagizo yote niliyopewa ya kujiunga na shule hii.
5. Historia fupi ya mwanafunzi husika. Jina kamili uliloandikis hwa shuleni Shule ya msingi na sekondari ulizopitia PICHA YA MWANAFUNZI Tareh e ya kuzali wa MSINGI: Mahali /Wilaya ulipozaliwa Dini /Dhehebu lako URAIA SEKONDARI:
6. Nakiri kuwa maelekezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi.

6.0 Jina kamili la mwanafunzi……………………………………saini…………….. tarehe…………………….

7 Sehemu ya mzazi/mlezi kukubali kuchaguliwa kwa mwanafunzi husika.

PICHA YA MZAZI/MLEZI

7.1Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………..Kazi……………………………………Kata mzazi anapoishi……………………………..kijiji /mtaa……………………. wilaya……………………. Namba ya simu ya mzazi / mlezi: ………………………S.L.P. …………………. Nakiri kuwa huyu ni mwanangu. Nakubali /Sikubali nafasi hii aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Nakubaliana / Sikubaliani na sheria na maagizo yote ya shule aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Naahidi kumuhudumia mwanangu kikamilifu na kushirikiana na uongozi wa shule katika kufanikisha maendeleo ya elimu yake. Sahihi ya mzazi/mlezi………………………………Tarehe……………………… *FUTA ISIYOHUSIKA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA**

**SHULE YA SEKONDARI KICHEBA**

**S.L.P 58, MUHEZA . SIMU: +255 686756071:**

# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**Medical Officer**

______________________________________________

______________________________________________

**Name of Student**____________________________________________________________

**Please examine the above-named student to ascertain his fitness for further studies.**

**Medical Certificate**

***(To be completed by Medical Officer)***

I have examined the above named with regard to:-

Skin…………………………………………………………………………………………

Eyes…………………………………………………………………………………………

Ears…………………………………………………………………………………………

Chest………………………………………………………………………………………..

Abdomen……………………………………………………………………………………

Urine………………………………………………………………………………………..

Stool………………………………………………………………………………………...

Hemoglobin…………………………………………………………………………………

And I considered

1. He is in good/not good healthy, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school
2. He is / is not now fit to return to school after having treatment for……………………………………………………………………………………...

…………………  ………………

**Name and signature of Medical Officer** **Date** **Stamp**

**PICHA ZA AINA NA RANGI YA KITAMBA CHA GAUNI LA SHAMBANI (Shamba Dress) na RANGI YA SWETA**



Kitambaa kwa ajili ya Shamba Dress



Rangi ya Sweta